SIGNAL Publishers

GREDI YA 7 - 2025

THE SCHOLAR
007

# SIGNAL CBE ASSESSMENT
# JARIBIO LA SABA

## JUNIOR SCHOOL ASSESSMENT

## — KISWAHILI KARATASI YA 2 —

**MUDA: SAA 1 DAK 30**

JINA: ..................................................

GREDI: ..................................................

SHULE: ..................................................

NAMBARI YA TATHMINI: ..................................................

**Maagizo kwa mwanafunzi:**

1. Andika jina lako, jina la shule yako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa.
2. Soma kila swali kwa makini
3. Mtahiniwa ahakikishe kuwa kurasa zote kwenye kijitabu hiki zimepigwa chapa.
4. Jibu maswali yote katika kijitabu hiki.
5. Nakili sahihi yako katika kiapo kilicho chini ya ukurasa huu.

**Kiapo: "Naapa kutokiuka sheria zozote wakati wa mtihani huu".**

**Sahihi:** .................................................. **Tarehe:** ..................................................

PREDICTIONS AVAILABLE

**SEHEMU YA A: KUANDIKA (alama 15)**

**Andika insha ya maelezo kuhusu;**

**UTUNZAJI WA MAZINGIRA SHULENI**

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

..........................................................................................................................................

## ZOEZI 2: FASIHI SIMULIZI. (Alama 20)

**Maswali**

(a) Andika tofauti kati ya nyimbo zifuatazo.

(i) Bembelezi na nyimbo za watoto (Alama 8)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(ii) Nyimbo za kazi na nyimbo za dini

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(b) Eleza sifa tatu za fasihi simulizi. (Alama 3)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

(c) Taja faida tatu za fasihi simulizi katika jamii. ( Alama 3)

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

***Soma wimbo ufuatao kisha ujibu maswali***

**CHAPA KAZI**

Chapa kazi
Chapa kazi
Nawe mkwezi
Kwea mnazi
Angua nazi
Chapa kazi

Chapa kazi
Chapa kazi
Mkulima
Chapa kazi
Shika jembe
Ng'oa magugu
Chapa kazi

Chapa kazi
Chapa kazi
Nawe mvuvi
Shika nyavu
Tosa majini
Chapa kazi

**Maswali**

(a) Wimbo huu ni wa aina gani? (Alama 1)

..................................................................................................................................

(b) Taja sifa moja ya nyimbo za aina hii inayojitokeza katika wimbo huu. ( Alama 1)

..................................................................................................................................

(c) Eleza shughuli mbili za kiuchumi ambazo jamii ya wimbo huu hushiriki. (Alama 2)

.....................................................................................................................

.....................................................................................................................

(d) Fafanua mambo mawili ambayo wawasilishaji wa wimbo huu wanaweza kufanya wanapoimba. (Alama 2)

.....................................................................................................................

.....................................................................................................................

**3. <u>NOVELA (Alama 15)</u>**

(a) Andika sifa tatu za novela. (Alama 3)

.....................................................................................................................

.....................................................................................................................

.....................................................................................................................

***<u>Soma sehemu ifuatayo ya novela kisha ujibu maswali</u>***

"Hodi huku! Hodi! Wenyewe mpo?" Bi. Makali alisikia sauti hiyo kwa umbali kutoka kwenye kochi ambako alikuwa ameketi akimngojea mwanawe. Ni sauti ambayo aliijua fika. Ni sauti ambayo alichelea sana kuisikia.

Bi. Makali alinyamaza jii. Alionekana kama mtu anayeushauri moyo wake kuitikia wito. Hakujua anyanyuke aende mlangoni kuufungua au aelekee chumbani mwa mwanawe kumkinga. Hatimaye busara ilimtuma kwenda mlangoni kumfungulia aliyekuwapo. Akilini aliwaza kwamba mtu hakatai wito hukataa aitiwalo. Mjumbe mara zote hauawi, hana hatia.

Bi. Makali alifungua mlango na kubaki amejishikilia kwenye fremu. Amini usiamini aliyebisha alikuwa Dina. Yeye na Dina walitazamana kama ndio wanakutana kwa mara ya kwanza. Nafasi iliyokuwa baina yao ilikuwa ndogo mno lakini walionekana wamebaidika kama ardhi na mbingu. Dina alimkazia macho Bi. Makali kana kwamba alitaka kujua kwa nini hampishi ndani. Kwa hakika karibu amwambie simile. Bi Makali naye alimtazama Dina kwa macho yaliyomuuliza "Kimekuleta nini huku baada ya siku zote hizi? Kwa nini unakuja kunivurugia mpango?"

Shangazi Dina alimtazama Bi. Makali huku amejawa na uoga. Alihofia kwamba huenda mama huyu alikuwa ameghairi nia. Baada ya muda alijutia huzuni ya mamba na kumjibu wifi yake huku akiangalia chini. "Pole sana wifi yangu sikukusudia kuwatia wasiwasi, nilikumbwa na matatizo fulani nilipoondoka hapo." Dina alisema haraka asije akangunduliwa kuwa anamdanganya wifi yake.

Mama Herina aliachilia kilio kikubwa ambacho kilimtahadharisha Herina kuwa siku ya siku ilikuwa imefika. Dina alijaribu kumpoza Bi. Makali akisema kwamba hata yeye alishangazwa na uamuzi wa mzee Makali. Hayo yote yalipitia kwenye sikio moja la Bi. Makali na kutokea kwenye sikio la pili. Mume wake hakuwahi hata siku moja kutaka kumuumiza yeye na wanawe. Itakuaje katika utuuzima wao aanza kumuumiza?

**<u>Maswali.</u>**

(a) Taja mandhari yanayojitokeza katika sehemu hii ya novela. (Alama 1)

.....................................................................................................................

(b) Taja wahusika wowote wawili katika sehemu hii ya novela. (Alama 2)

.....................................................................................................................

(c) Eleza sifa moja ya Dina inayodhihirika katika sehemu hii ya novela. (Alama 2)

.....................................................................................................................

.....................................................................................................................

(d) Ni mbinu zipi za lugha zilizotumiwa katika kauli zifuatazo: (Alama 4)

(i) Alinyamaza jii ......................................................

(ii) Anayeshauri moyo wake ......................................................

(iii) Mtu hakatai mwito hukataa aitwalo......................................................

(iv) Wamebaidika kama ardhi na mbingu ......................................................

(e) Kwa nini Dina alimtazama Bi Makali kwa uoga? ...................................................... (Alama 1)

(f) Huenda uhusiano kati ya Dina na Bi. Makali haukuwa mzuri. Thibitisha haya kwa kutolea maelezo kutokana na sehemu hii ya novela. (Alama 2)

.....................................................................................................................

.....................................................................................................................